

Tunatoa ushauri

Jumatatu-Ijuma saa tatu-saa mnane

(Siku ya kwanza-Siku ya tano saa tatu-saa mnane)

Kidenishi na Kiingereza
Simu 33 73 50 00

Kwenye nambari zifuatazo tuna towa ushauri
– Zaidi ya Kidenishi – pia kwa lugha ya

Kibosnia / Kiserbia / Kikroeshia
Simu 33 73 52 33

Kiarabu na Kikurdi (sorani)
Simu 33 73 52 28

Kisomalia
Simu 33 73 53 11

Kiurdu na Kipunjabi
Simu 33 73 52 05

Ikiwa unataka ushauri kamili wa mtu binafsi
kuhusu haki zako kuhusiana na kurudi, lazima ujaze fomu ya habari, ambayo
unaweza kupata kwenye tovuti yetu.

www.atvendehjem.dk

Unaweza pia kutuandikia kwa
atvendehjem@drc.ngo



KUHUSU KURUDI INCHINI 2024

**Habari kwa ajili ya wakimbizi, wahamiaji na raia
wa nchi mbili juu ya kurudi kwa hiari..**

IKIWA UNAWAZA KURUDI NYUMBANI

Baraza la Wakimbizi la DRC la Denmark linatoa ushauri kwa raia kurejea kwa hiari katika nchi yao ya asili, nchi ya makao ya zamani au nchi ambayo kuna uhusiano wa karibu wa kifamilia. Wakimbizi, wahamiaji na watu wenye uraia wa nchi mbili (mmoja wa Denmark na uraia mwingine) wana fursa ya kupokea msaada wa kifedha ikiwa wanarudi nyumbani. Ikiwa unaweza kupokea usaidizi inategemea wakati gani ulifika Denmark na ni aina gani ya kibali cha makao ulicho nacho.

Iwapo ungependa kujua kama unaweza kupata usaidizi wa kurudi katika nchi yako, tutumie fomu ya taarifa katika www.atvendehjem.dk.

MSAADA WA KIFEDHA

Mnamo mwaka wa 2024, watu wazima wana fursa ya kupokea hadi DKK 155.417 ili kuanza maisha mapya katika nchi yao ya asili. Watoto wana fursa ya kupokea hadi DKK 47.401.

Pesa hulipwa katika sehemu mbili - sehemu ya kwanza wakati wa kuondoka (unapewa kiasi ya DKK 62.166 kwa watu wazima, kiasi ya DKK 18.960 kwa watoto) na sehemu ya pili (kiasi ya DKK 93.251 kwa watu wazima, kiasi ya DKK 28.441 kwa watoto) hulipwa nje baada ya mwaka mmoja katika nchini nyumbani kwako.

FURSA ZA MSAADA WA ZIADA

- Msaada ya usafiri,
- Usafirishaji wa mali au usaidizi kwa gharama za ununuzi wa mali ya kibinafsi;
- Vifaa vya biashara na usafirishaji wa vifaa vya biashara,
- Gharama za bima ya afya/matibabu kwa miaka nne,
- Dawa kwa mwaka mmoja wa matumizi,
- Misaada zingine za lazima,
- Malipo ya shule kwa miaka 4 kwa watoto wa miaka 5 -16;
- Msaada wa upataji wa hati za kusafiria.

IKIWA UNA MIAKA 55

Ikiwa una angalau umri wa miaka 55 unaporudi nyumbani, unaweza pia kulipwa kiasi fulani cha usaidizi kutoka Denmark kila mwezi.

Ikiwa una umri wa kati ya miaka 50 na 54, unaweza kulipwa kiasi hicho katika hali maalum.

Usaidizi kwa kawaida huwa kati ya DKK 2,800 na DKK 3,600 kwa mwezi. Ili kupokea usaidizi, lazima uwe na kibali cha kuishi nchini Denmark kwa angalau miaka 5.

Iwapo kuna makubaliano ya nchi mbili kati ya Denmark na nchi yako ya asili, inawezekana kuchukua sehemu ya pensheni yako nawe.

HAKI YA KUBADILI MAONI

Wakimbizi wana haki ya kubadili uamuzi wa kurudi nyumbani na kuja tena Denmark mu muda ya mwaka mmoja. Kwao, hii ina maanisha kwamba wanaweza tena kupata kibali cha kukaa nchini Denmark. Hata hivyo, ni lazima walipe msaada wote wa kuwarejesha inchini mwao ikiwa watabadili maoni yao ya kurudishwa kwao.

Wahamiaji hawana haki ya kurudi Denmark wanapokuwa wamesafiri na wamepata usaidizi wa kurejea nchini mwao. Kwao, uamuzi huo ni wa mwisho na kwaheri kwa haki ambazo wamekuwa nazo wakati wa kukaa kwao nchini Denmark.

Raia wa nchi mbili lazima wanyime uraia wao wa Denmark kwa kiasi kabla ya kuondoka. Wana nafasi ya kubadili maoni wa kutoa uraia wa Denmark kwa miaka miwili. Iwapo watabadili kurudishwa nyumbani, lazima walipe msaada wote waliopewa wa kuwarudishwa nyumbani.

UKITAKA KUJUA ZAIDI

Ikiwa unafikiria kurudi katika nchi yako, unaweza kututumia fomu ya habari, ambayo unaweza kupata kwenye tovuti yetu. Katika mahojiano ya mtu binafsi, tunakujulisha kuhusu chaguo na haki zako ili uweze kufanya uamuzi wako. Tunatoa mkalimani kwa mahojiano ukipenda. Kazi yetu ni kukupa habari unayohitaji ile ufanye uamuzi wako.